HOTUBA YA MHE. MOHAMED CHANDE OTHMAN, JAJI MKUU WA TANZANIA, YA KUMKARIBISHA MGENI RASMI, MHE. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (Mb), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUFUNGUA MKUTANO WA WAH. MAJAJI, TAREHE 12-13, NOVEMBA, 2012, SNOW CREST HOTEL, ARUSHA

Mh. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Wah. Majaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania,

Mh. Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Zanzibar,

Mh. Fakihi R. Jundu, Jaji Kiongozi,

Wah. Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania na ya Zanzibar,

Mh. Magesa Mulungo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha,

Mh. Gaudence Lyimo, Meya wa Jiji la Arusha,

Ndugu Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutukusanyisha hii leo. Wengi wetu tumelazimika kusafiri mwendo mrefu kuja kwenye mkutano huu wa Waheshimiwa Majaji unaofanyika hapa Arusha. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, safari hizo zilikuwa za salama.

Aidha naomba kuchukua nafasi hii kuwakaribisha tena Waheshimiwa Majaji wote, kwenye Mkutano huu wa Majaji wa Mahakama ya Tanzania. Ninasema, karibuni wote hapa Arusha. Mara ya mwisho tulikutana tarehe 24-26 Mei, 2010, takriban miaka miwili na nusu iliyopita.

Mhe. Waziri Mkuu, kwa heshima na taadhima naomba, kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wangu kuwa Mgeni Rasmi kwenye ufunguzi wa Mkutano wa Waheshimiwa Majaji wa Tanzania mwaka huu, 2012. Kazi zako nyingi za kulitumikia taifa letu zingekuwa sababu tosha kwako za udhuru wa kutokubali mwaliko wangu. Na tungekuelewa kabisa. Kukubali kwako ni ushahidi wa jinsi unavyoipa thamani Mahakama ya Tanzania wake katika kutekeleza na kusimamia utawala wa sheria hapa nchini. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya Mahkama ya Tanzania ninashukuru sana.

Mhe. Waziri Mkuu, kwa nafasi hii pia ninawashukuru Viongozi wa Mkoa na Jiji la Arusha kwa kuweka mazingira yaliyowezesha mkutano huu kufanyika katika hali ya usalama na utulivu mkubwa. Ninawashukuru sana.

Mhe. Waziri Mkuu, Mahakama ya Tanzania siku zote inatambua mchango wake katika maendeleo, amani na utawala bora wa nchi yetu. Kwa kuzingatia hilo, madhumuni ya mkutano wa Wah. Majaji mwaka huu ni :

1. Kuchambua na kutathmini kwa pamoja hali halisi ya utoaji haki na mashauri katika ngazi za Mahakama ya Tanzania;
2. Kuainisha mikakati mipya na mipango maalum ya kuharakisha usikilizaji wa mashauri;
3. Kuainisha vipaumbele vya Mahakama miaka mitano ijayo, yaani 2013-2017; na
4. Kutambua na kuboresha uendeshaji wa Mahakama na huduma kwa wananchi zinazotolewa na Mahakama.

Mhe. Waziri Mkuu kama utangulizi, kwa sasa na kama hesabu uwezo wa Mahakama kwa ujumla wa kutoa haki ni kuamua takriban idadi ile ile ya mashauri yanayowasilishwa Mahakamani kwa mwaka ule. Suala lilobaki ni Lile la kushughulikia kikamilifu mashauri yaliyodumu zaidi ya miaka miwili, Ambayo ndiyo kiini cha msongamano wa mashauri Mahakamani. Tutatumia fursa ya mkutano huu kuandaa majibu mapya ya hali hiyo kwenye Mahakama zetu.

Pamoja na hayo, Mhe. Waziri Mkuu ili Mahakama iweze kutenda haki, ni lazima Watanzania wapate fursa ya kupata haki. Mahakama pia inabidi ijijengee heshima na imani ya wananchi. Haiwezi kulazimisha kuheshimiwa. Hilo ni jepesi kufikiwa ikiwa Mahakama itatoa haki kwa wote na kwa wakati. Tunajua kuwa wengi, haswa wenye mashauri yao Mahakamani hutupima kwa kuzimaliza kesi, na sio kwa kuanza kesi.

Mhe. Waziri Mkuu, Mahakama ya Tanzania inafuraha kubwa kuona kuwa, ***kwanza,*** kuna ongezeko muhimu la mashauri yanayoletwa Mahakamani na wananchi. Ongezeko hilo ni katika ngazi zote za Mahakama na hasa zile za chini, yaani Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi. Hili linadhihirisha kuwa wananchi wana uelewa wa haki zao na vile vile wana fursa ya kudai haki zao. Kwa sababu hiyo Mahakama inawajibika kukidhi mahitaji ya utoaji haki.

Pili, aidha kwa mwaka 2009 na 2010, upo mwelekeo wa jumla unaoonesha kupungua kwa idadi ya mashauri ambayo hayajasikilizwa katika Mahakama zote. *Tatu,* theluthi mbili ya mashauri yote yaliyoko Mahakamani yako katika Mahakama za Mwanzo. Juhudi zetu inabidi zilenge pia ngazi hii ya Mahakama ambayo ndiyo inatoa haki na huduma kwa Watanzania wengine na nchi nzima.

Nne, Mhe. Waziri Mkuu, kama unavyoona tunataka kuchukua nafasi hii ya kuwa pamoja sio tu kutathmini na kujipima, bali pia kuandaa mikakati na mipango mipya ya kuboresha utoaji haki. Tunafahamu fika kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kwenye Ibara ya

107A(1) kwa kuitambua Mahakama kama ndiyo chombo cha mwisho cha utoaji haki. Tunakubali na kutambua kuwa hiyo ni dhamana nzito.

Mhe. Waziri Mkuu, katika kujipanga kutoa haki tutazingatia kuwa Mahakama pia ni watoa huduma kwa jamii, huduma hiyo - haki, inabidi itolewe kwa uwazi, bila ya kucheleweshwa kwa sababu zenye kutiliwa shaka, kwa usawa, kwa gharama nafuu kwa mwananchi, na kwa kuto kuzingatia sana ufundi wa sheria, bali kutia maanani haki ya msingi. Ahadi yetu kwa wadau wa Mahakama inasema hivi: ***tunataka uhai wa shauri la aina yoyote liletwalo Mahakamani usizidi miaka miwili.*** Hilo tunaliigania. Hatutaki kuendelea kuwa mateka wa msongamano wa mashauri. Mhe Waziri Mkuu, kupitia kwako, tunaiomba Serikali katika ngazi zote, iendelee kushirkiana nasi kufanikisha utoaji haki unaoridhisha wote.

Mhe. Waziri Mkuu, kama unavyofahamu, kutokana na taaluma na waledi wa kazi walizonao Waheshimiwa Majaji na Mahakimu, ninayo matumaini kuwa malengo ya mkutano huu yatafanikiwa kwa ufanisi mkubwa. Tukiongozwa na Dira yetu yaani, ***"Kutoa Haki Sawa kwa Wote na kwa wakati"*** bila shaka, yote yatakayojadiliwa na kuamuliwa katika mkutano huu yatakuwa chachu ya mabadiliko chanya katika ngazi zote za Mahakama hapa nchini. Tunatoa ombi kwa wadau wetu wote, kila mmoja kwa nafasi yake, watuunge mkono katika juhudi hizi.

Mhe. Waziri Mkuu, kama nilivyosema hapo awali, tunayo bahati kubwa ya kuwa na wewe hii leo, ili utufungulie mkutano wetu. Ni heshima yangu kwako, baada ya maneno haya machache, kukukaribisha.